OUKA
Osaka University Knowledge Archive



| | |
|---|---|
| Title | Utamaduni wa Kiswahili Juu ya Mambo yahusuyo Dini, Chakula, na Desturi za Mavazi |
| Author(s) | Isack, Zainabu Kassu |
| Citation | 外国語教育のフロンティア. 2020, 3, p. 193-205 |
| Version Type | VoR |
| URL | https://doi.org/10.18910/75635 |
| rights | |
| Note | |



*Osaka University Knowledge Archive : OUKA*

https://ir.library.osaka-u.ac.jp/

Osaka University

# Utamaduni wa Kiswahili Juu ya Mambo yahusuyo Dini, Chakula, na Desturi za Mavazi

## Swahili Culture on Aspects Related to Religion, Food, and Dressing norms

ISACK, Zainabu Kassu

**Abstract**

The aim of this brief article is to highlight on three more aspects of Swahili Culture under the title: *Utamaduni wa Kiswahili Juu ya Mambo yahusuyo Dini, Chakula, na Desturi za Mavazi (Swahili Culture on Aspects Related to Religion, Food, and Dressing norms)*. We repeat (a quote from our previous articles) for emphatic purpose that, we define Culture as the sum total of social behaviours, traditions, customs and a total way of life of a particular society. Culture looks at the regular practices of the given society such as; when or what they eat, their dress codes, greetings, their etiquettes, taboos, their beliefs and so on (Isack 2018:105, Isack 2019:259). In the previous work under the tittle; *Dhana na Dhima ya Familia na Unasaba katika Utamaduni wa Kiswahili* (Isack 2019) we recommended that in order to enrich knowledge on Swahili Culture and African Culture at large it is important to discuss more aspects in our literatures. We also emphasize that still there are challenges in the instruction of Swahili Language and its Culture to foreign learners due to the lack of enough reference materials designed for them (Isack 2018:105). Both instructors and learners of Swahili as a foreign language can benefit from this work and thus narrow the current knowledge gap.

Keywords: Dini, Chakula, Mavazi, Utamaduni wa Kiswahili

**Iksiri**

Lengo la makala hii fupi ni kuangazia vipengele vitatu zaidi vya utamaduni wa Kiswahili kupitia mada: *Utamaduni wa Kiswahili Juu ya Mambo yahusuyo Dini*, *Chakula, na Desturi za Mavazi*. Tunakariri (nukuu kutoka makala mbili zilizotangulia) kwa lengo la kusisitiza kwamba; Tunaufasili utamaduni kama ni jumla ya tabia, mila, desturi na mitindo ya maisha ya watu wa jamii fulani. Utamaduni unaangalia namna watu wanavyofanya mambo yao kwa kawaida kama vile; wakati gani au nini wanakula, mavazi yao, wanasalimiana vipi, mambo ambayo ni adabu, miiko yao, mambo wanayoamini n.k (Isack 2018:105, Isack 2019:259). Katika makala iliyopita yenye mada; *Dhana na Dhima ya Familia na Unasaba katika Utamaduni wa Kiswahili* (Isack 2019)

tulipendekeza kuwa katika maandiko yetu, ni muhimu kuendeleza juhudi za kujadili vipengele vingine vinavyoutambulisha utamaduni wa Kiswahili ili kutajirisha maarifa juu Utamaduni wa Kiswahili na Utamaduni wa Kiafrika kwa ujumla. Tunarudia tu kutaja pia kuwa, bado kuna changamoto katika ufundishaji wa Lugha ya Kiswahili na Utamaduni wake kwa wanafunzi wageni kutokana na uhaba wa rejea zinazowalenga wajifunzaji wageni (Isack 2018:105). Makala hii inaweza kuwanufaisha wakufunzi na wajifunzaji wa Kiswahili kama lugha ya kigeni na hivyo kupunguza mwanya wa maarifa uliopo hivi sasa.

## 1. Utangulizi

Makala hii imegawanyika katika sehemu kuu tano (5); Sehemu ya kwanza ni utangulizi unaolezea mpangilio wa makala hii. Sehemu ya pili inazungumzia mambo yanayohusiana na dini hususan dini ya Kiislamu, pia inagusia itikadi nyingine (superstitions) ambazo hazihusiani na dini ya Kiislamu ambazo zipo katika utamaduni wa Kiswahili. Sehemu ya tatu (3) tunazungumzia mambo mbali mbali kuhusu chakula kama vile majina ya vyakula, namna za mapishi na mambo ya kitamaduni kuhusiana na chakula ikiwemo adabu na miiko ya chakula. Katika sehemu ya nne (4) tunazungumzia desturi za mavazi kwa kuzingatia jinsia, rika na urasmi. Pia mambo ya adabu na yale yasiyofaa kitamaduni kwa upande wa mavazi. Mwishowe tunafafanua juu ya khanga, vazi maarufu linaloutambulisha utamaduni wa Waswahili hasa sehemu za Afrika ya Mashariki. Sehemu ya tano (5) na ya mwisho ni hitimisho; katika sehemu hii tunatoa muhtasari wa makala hii na mapendekezo kwa makala zijazo.

## 2. Mambo yahusuyo Dini

Dini ni kipengele kingine kinachoweza kuutambulisha utamaduni wa watu. Kamusi ya Kiswahili Sanifu (2014) inafasili dini kama "imani inayohusiana na mambo ya kiroho kwamba kuna muumba ambaye aliuumba ulimwengu huu na kwamba ndiye mtawala wa kila kilichomo". Pia, kamusi hiyo inafasili dini kama "mfumo fulani wa imani hii na njia ya kuabudu, kusali na kuheshimu/ kutii huyo muumba". Kwa ujumla tunaweza kusema dini ni jumla ya imani za binadamu pamoja na mafundisho kuhusu mambo ambayo watu wanayazingatia na kuamini, yaani mambo ya roho kama vile mambo kuhusiana na Mungu, maisha na uumbaji. Mifano ya dini kuu duniani ni kama Uislamu, Ukristo, Ubudha, Uyahudi na Uhindu. Hata hivyo, Afrika pamoja na dini hizo kuu zipo dini na itikadi nyingine za kiasili.

Kwa upande wa Waswahili, mtu anapoulizwa Mswahili ni nani? Unaweza kusikia majibu kama; Mswahili ni mtu anayesema Kiswahili, mtu wa pwani, na Mwislamu. Mbaabu (1985) katika utangulizi wa kitabu chake anawaelezea Waswahili kama ifuatavyo, "Waswahili ni wafuasi wa

dini ya Kiislamu. Wao ni wacha Mungu na ni watu wanaojitahidi kutenda mema mbele ya Mungu na binadamu wenzao. Waswahili huthamini tabia njema ya watoto wao na hufanya kila jitihada kuwafunza watoto wao kutenda mema". Waswahili kwa kawaida wananasibishwa sana na Uislamu, na swali la kujiuliza ni kwa nini? Na hakika sababu ya jambo hilo ni ya Kihistoria.

Kihistoria wenyeji wa sehemu za pwani ya Afrika Mashariki wenye asili ya Kibantu waliathiriwa na ujio wa Waarabu ambao walikuwa Waislamu. Neno "Sahel" ni neno la Kiarabu na maana yake ni Pwani. Kwa hivyo, jina la "Waswahili" yasemekana ni jina lenye asili ya Kiarabu kutokana na jina walilotumia Waarabu kuwaita wakazi/wenyeji hao wa pwani yaani "sawahila". Na vivyo hivyo, "Kiswahili" ni lugha ya wakazi hao wa pwani. Waswahili wenyewe walijitambulisha kwa majina ya makabila yao kama vile Wakilindini au Wamrima.

Waarabu waliingia pwani ya Afrika Mashariki kufanya biashara mapema kabla ya ujio wa wakoloni na wageni wengine kama Wareno, Wajerumani, na Waingereza. Maeneo waliyoingia ni pamoja na; Mombasa, Tanga, Dar es Salaam, na Kilwa. Waarabu wa kutoka Yemen ndio waliokuwa wengi kuliko wale wa Oman. Waarabu wa Oman, hata hivyo walitawala Zanzibar miaka ya 1800. Waarabu wa Yemen walijenga misikiti, kuwasilimisha na kuwafundisha Uislamu wakazi/ wenyeji kila mahali walipopita na kukaa kufanya biashara. Biashara zao zilikuwa kama vile biashara ya karafuu, biashara ya utumwa na biashara ya meno ya tembo.

Hivyo utamaduni wa Kiswahili umefungamana kwa kiasi kikubwa na dini ya Kiislamu, kiasi kwamba hatuwezi kuzungumzia utamaduni huo bila kuzungumzia dini ya Kiislamu. Kama asemavyo Mbaabu (1985:6), "Karibu Waswahili wote ni wafuasi thabiti wa dini ya Kiislamu. Kwa kuwa wamekuwa na dini hiyo kwa karne nyingi, maisha kwa jumla, ushirikina, ndoa na kadhalika yamefungamana sana na Uislamu hivi kwamba ni vigumu kuyatenganisha. Kwa hivyo ni dhahiri kwamba itikadi na desturi zote za Waswahili haziwezi kuzungumziwa kwa undani bila kugusia dini ya Kiislamu".

### 2.1 Je, misingi ya Uislamu ni ipi?

Waislamu kwa ujumla wanaongozwa na nguzo tano muhimu (*arkanul-islaam*). Nguzo hizi ni ibada au matendo yanayoaminiwa kuwa ya msingi katika Uislamu duniani pote. Katika sehemu ifuatayo tutafafanua kwa ufupi nguzo hizo.

### 2.2 Nguzo ya Kwanza: Shahada

Shahada au kushahadia yaani kukubali kwa moyo na kukiri kwa ulimi kuwa hapana Mola apasaye kuabudiwa kwa haki ila Allah na kuwa Muhhammad ni mtume wa Mwenyezi Mungu (*Ashahadu An-laa ilaha illa llah wa ash ahadu anna Muhhammadan rasulu llah*). Waislamu

wanaamini kuna Mungu mmoja tu, naye hakuzaa wala hakuzaliwa na pia Mungu hana mfano wake katika dunia. Na hivyo miongoni mwa dhambi kubwa katika Uislamu ni kuamini/ kuabudu kitu kingine kisichokuwa Mwenyezi Mungu ("*shirk*" yaani ushirikina). Na kisha baada ya kumuamini Mungu mmoja sharti ushuhudie kuwa Muhhammad ni mtume/mjumbe wa Mungu na hivyo kufuata mafunzo aliyoyaleta kwa umma wake. Shahada hizi mbili ndio sharti la msingi kwa mtu yeyote anayetaka kuingia katika Uislamu yaani *kusilimu*.

### 2.3 Nguzo ya Pili: Swala

Waislamu wanaamini kuwa sababu ya kuumbwa/kuletwa duniani ni kumuabudu Mungu. Kwa hivyo, kila siku ni sharti kuswali mara tano. Nyakati za swala hizo pia ni nyakati maalumu. Swala ya kwanza, ni swala ya *Alfajiri*. Swala hiyo husaliwa kunapoanza kupambazuka lakini kabla jua la asubuhi kuchomoza nayo huswaliwa kwa *rakaa* mbili. Swala ya pili ni swala ya *Adhuhuri*. Swala hiyo huswaliwa mchana, aghalabu jua linapokuwa kati kati nayo ni rakaa nne. Swala ya tatu ni swala ya *Alasiri*, hii huswaliwa pindi jua linapopita nusu lakini kabla halijazama/halijatua nayo ni rakaa nne. Swala ya nne ni swala ya *Magharibi* hii huswaliwa pindi wekundu wa jioni unapoingia/ jua linapozama nayo ni rakaa 3. Na swala ya mwisho ni swala ya *Ishaa* hiyo huswaliwa giza/ usiku unapoingia nayo ni rakaa nne. Swala ina utaratibu maalumu kama namna ya kusimama, kuinama (*kusujudu au kurukuu*), maneno ya swala, idadi ya rakaa n.k. Pia, ni sharti la msingi mtu kutawadha/kuchukua udhu (kujiweka safi/tohara) kabla ya swala pamoja na kuwa na mavazi safi yasiyo na najisi (uchafu) kama vile damu, mkojo au usaha, kuswali katika mahali pasafi pia ni muhimu. Swala ni faradhi (lazima) kwa Mwislamu yoyote aliyefikia balehe isipokuwa kwa dharura maalumu kama vile kwa wanawake wanapokuwa katika hedhi au katika damu ya nifasi (uzazi) hawaruhusiwi kuswali pamoja na ibada nyingine mpaka wanapomaliza na kuoga kujitoharisha.

### 2.4 Nguzo ya Tatu: Zakka

Nguzo hii inawahusu watu wenye mali inayowajibika kutolewa zakka nayo ina masharti maalumu kama vile mali iwe imefikia kiwango maalum kisharia (*niswaab*), yenye umiliki timamu (*milki taam*) na iliyopita mwaka (*hawalaani hawl*). Zakka ni uwanja mpana wa kisharia na hatutaingia kiundani hapa. Zipo zakka za aina mbali mbali ikiwemo zakka ya dhahabu na fedha, zakka ya pesa, wanyama, matunda na mazao n.k. Ibada hii inalenga kuwasaidia maskini au Waislamu wasiojiweza ili nao waweze kuishi vizuri. Kujenga uhusiano mzuri katika jamii kwa kusaidiana. Kupunguza tofauti kati ya maskini na matajiri kwa kuweka mzunguko wa mali na kufanya makundi ya watu masikini kupata rasilimali, kama namna ya kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa watu wenye mali kutoa mali hiyo kwa ajili ya kutekeleza ibada waliyoamrishwa na

Mungu n.k. Vile vile zipo mali ambazo hazifai/haziwajibiki kutolewa zakka kama vile mali ya haramu (kama ile ya wizi, riba, rushwa, na unyang'anyi), mali ya serikali kwani haina mmiliki aliyekamilika, mali zilizowekwa wakfu kwa kundi kubwa maalumu kama mayatima, misikiti au madrasa.

**2.5 Nguzo ya Nne: Saumu (mfungo)**

Yaani kufunga katika mwezi mtukufu wa Ramadhani. Hii ni nguzo nyingine muhimu kwa Waislamu. *Ramadhani* ni jina la mwezi mmojawapo katika majina ya miezi katika kalenda ya Kiislamu (Hijria). Katika mwezi huu inaaminika kitabu cha *Kurani* kiliteremshwa kwa Mtume Muhhammad (Rehema na amani ziwe juu yake). Na pia, ni faradhi (sharti) kwa Waislamu wote (watu wazima) kufunga kwa siku 29/30 kulingana na mwandamo wa mwezi, isipokuwa kwa wagonjwa, walio safarini au walioharamishiwa kufunga katika vipindi maalum kama wanawake walio katika hedhi au nifasi. Hata hivyo, ikiwa mtu amekosa kufunga kwa dharura moja wapo kama zilizotajwa, ni sharti kufunga siku alizoacha kabla ya kuingia Ramadhani nyingine au kutoa fidia kwa kuzingatia sharia.

**2.5.1 Je, kufunga ni nini? Na kuna maana/faida gani?**

Katika imani ya Kiislamu kufunga ni kuacha kula na kunywa na mambo ambayo ni halali kama vile kujamiiana (kwa wanandoa) kutoka inapoingia Alfajiri hadi Magharibi. Lakini, pamoja na kuacha hayo, kufunga ni kuzidisha ibada/kufanya mambo mema na kuacha kabisa mambo yote mabaya. Na watu wanapofunga wanatarajiwa kujifunza uvumilivu na kufikiri juu ya watu wenye taabu na wasioweza kupata chakula. Mafunzo hayo, bila shaka yatawafanya wawe watu bora zaidi. Pia, kufunga kunaaminika humpa mtu afya. Zaidi, Waislamu wanaamini kuwa mwezi huo ni mtukufu, na watu wanapotubu na kuomba husamehewa na kupata baraka na kujibiwa maombi yao.

Mwisho wa mfungo ni sherehe. Sherehe hiyo huitwa *Idd-l- Fitri* (Idi ndogo). Katika Idi hii watu wenye uwezo wana sharti la kutoa zakka (zakka ya fitri) kwa masikini kabla ya swala ya Idi. Maana yake ni kuwafanya watu masikini nao washerehekee sikukuu hiyo kama watu wenye uwezo. Halafu, watu huswali swala ya Idi, hula na kunywa na kutembelea jamaa na marafiki.

**2.6 Nguzo ya Tano: Kuhiji Makka**

Nguzo hii pia inawahusu watu wenye uwezo wa mali na afya kwa mujibu wa sharia kwenda kuhiji mahali patakatifu *Makka* walau mara moja katika uhai wao. *Hijja* hufanyika katika msimu maalumu aghalabu siku ya 8-13 katika mwezi wa *Dhulhaji*, mwezi wa mwisho katika kalenda ya Kiislamu. Idd l-haji ni siku ya kumi katika mwezi wa Dhulhaji na inasherehekewa na Waislamu

kote duniani kwa swala ya Idi na ni sunna kuchinja mnyama kama mbuzi, kondoo au ngamia. Matendo wanayofanya *mahujaji* katika ibada ya hijja ni pamoja na *kuhirimia* (kuweka nia na kuvaa mavazi ya hijja), *kutufu* yaani kuzunguka Kaaba (jengo tukufu lililopo Makka na uelekeo wanaoelekea Waislamu wanaposwali), kutembea mara 7 katika ya vilima vya Safa na Marwah na kisha kunywa maji ya kisima cha Zamzam, kusimama Arafa (mlima Arafa) na kwenda kulala Muzdalifa, kufanya ishara ya kumtupia mawe shetani katika viguzo vitatu (*jamaraat*) na kunyoa/ kupunguza nywele baada ya kutoa kafara ya kuchinja mnyama. Hekima ya ibada ya hijja ni kuonyesha unyenyekevu kwa Mola kwa kutimiza ibada iliyoamrishwa naye na kuweza kukutana kwa Waislamu wa dunia nzima na kudhihirisha kuwa watu wote ni sawa pasi na kujali hadhi ya mtu, rangi, utaifa au lugha. Zaidi, kijamii mtu aliyekwenda hijja tayari hupewa cheo cha Alhaji (mwanamume) na Hajja/Hajati (mwanamke) na maana yake ni "aliyehiji". Unaweza kusikia cheo hiki kikiambatanishwa na jina la muhusika kama vile Alhaji ali Hassan Mwinyi (aliyekuwa raisi wa pili wa Tanzania).

**2.7 Athari ya dini katika Maisha ya Waswahili**

Pamoja na nguzo 5 za Uislamu tulizozizungumzia katika sehemu iliyotangulia, Waislamu wana nguzo sita za Imani (*arkanul-imaan*) ambazo ni; Kuamini Mungu mmoja tu na Malaika wake (kama vile; Jibrili, Mikaili, Izraili, na Israfili), vitabu vyake (Kurani na vitabu vingine vilivyoteremshwa kabla yake kama vile Taurati, Zaburi, na Injili), kuamini mitume wake (Mtume Muhammad rehema na amani iwe juu yake na mitume wengine walioletwa kabla yake kama vile nabii Musa, Isa na Daudi), kuamini siku ya Kiama (siku ya malipo) na kuamini Kadari (*qadar*) yake ya kheri au ya shari.

Maisha ya Waswahili yamefungamana sana na misingi hii ya dini ya Kiislamu. Tunaweza kusema kuwa kwa Waswahili wa kweli maisha yao yote huongozwa na dini tangu kuzaliwa mpaka anapoingia kaburini (kufa). Waswahili na Waislamu kwa ujumla, wanaamini kuwa tuliumbwa na Mungu, na tupo hapa duniani ili kumuabudu Mungu. Na kuwa, maisha ya duniani ni maisha mafupi na ya kupita, si maisha ya milele. Maisha ya milele au makazi ya milele ni kwa Mungu/ maisha ya akhera. Unaweza kuona falsafa hiyo ya maisha katika misemo mbali mbali ya Kiswahili kama vile; "Duniani tunapita" au "Maisha ni safari"; safari hiyo inaanzia kwa Mungu, kisha duniani na mwishowe tunarejea kwa Mungu.

Waswahili/Waislamu wanaamini kuna siku ya mwisho, siku hiyo ni siku ya Kiama. *Kiama* ni mwisho wa maisha ya dunia na kila kitu kitafika mwisho wake, na watu/viumbe wote watafufuliwa na watakusanyika/kusimama mbele ya Mungu na wataulizwa juu ya yale waliyofanya duniani. Siku hiyo pia, huitwa siku ya malipo/siku ya hukumu. Kwa nini siku ya malipo/ siku ya hukumu?

Inaaminiwa kuwa namna mtu anavyoishi sasa duniani yaani amali zake ndiyo kipimo au mizani ya malipo yake katika maisha ya kesho akhera (maisha ya milele). Yaani, ikiwa mtu ataishi vizuri duniani kwa kumcha Mungu yaani kutenda aliyoamrishwa na Mungu na kuacha aliyokatazwa basi yeye atakuwa mtu mwema, na ataandikiwa thawabu (malipo mema) na siku ya Kiama basi ataingia peponi. Na ikiwa mtu ataishi vibaya duniani kwa kutenda maovu basi ataandikiwa dhambi (maasi) na atapewa hukumu ya kuingia motoni siku ya kiama.

Kwa ujumla, Waswahili wanaamini katika kudra za Mungu. Wanaamini maisha ya kila mwanadamu yameshaandikwa na Mungu, na kila jambo ambalo mtu hupata au hupitia ni kwa uwezo wa Mungu. Katika maisha ya kila siku ni kawaida kusikia kila jambo likihusishwa na Mungu. Kwa mfano: watu wanapokuwa na afya au wanapopata neema au mafanikio kama kupata kazi, mali, au watoto wanasema "ninamshukuru Mungu", wanapokuwa wagonjwa wanamwomba Mungu awaafu, wanapopitia jambo gumu wanasema “Mungu kanipa mtihani” na wanamwomba Mungu waushinde mtihani huo, mtu anapokufa, watu wanasema "hiyo ni kazi ya Mungu" au “tuliumbwa naye na kwake tutarejea” (*inna lillah wainna ilayhi rajiuun*). Hivyo, watu huomba Mungu kwa mambo mbali mbali kama kuwa na afya, kufaulu, kupata kazi, kupata pesa, kuepushwa na mambo mabaya n.k.

**2.8 Itikadi nyingine**

Hata hivyo, pamoja na imani hizo zinazoongozwa na misingi ya dini ya Kiislamu, Waswahili wana imani nyingine ambazo hazihusiani na dini ya Kiislamu. Tutazame mifano hii;

- Mtu anapokula chakula au kunywa kitu halafu akapaliwa au kujing'ata watu husema mtu huyo anatajwa/anasemwa vibaya.
- Mtu anapotembea na akajikwaa mguu wa kulia, watu huamini anapoenda pana heri, na ikiwa atajikwaa mguu wa kushoto basi anapoenda hapana heri naye.
- Bundi: Bundi anaaminika ni mwenye kuleta balaa, ikiwa bundi atalia karibu na nyumba ya mtu au katika paa la nyumba basi mtu huyo atapatwa na msiba.
- Paka mweusi: Paka mweusi pia ni ishara ya mkosi, ikiwa mtu atakutana na paka mweusi asubuhi, basi inaaminiwa siku hiyo ni yenye mkosi, huenda jambo baya litamtokea.
- Mama mjamzito kula mayai: Inaaminika kuwa ikiwa mwanamke mjamzito atakula mayai, basi atapata mtoto asiye na nywele.
- Kumpitia mwanamke mjamzito na moto ni mwiko mkubwa kwani inaaminiwa ni kumkata uzazi.
- Mama akikuvulia nguo: Ikiwa mama yako atakukasirikia na kukuonyesha sehemu za siri za mwili wake na huku akisema maneno ya kukulaani basi inaaminiwa utapatwa na laana hiyo na

huenda ukawa na maisha mabaya mbeleni au hata kuharibikiwa akili (wendawazimu).

- Kula gizani: mtu anayekula gizani basi anakula na shetani.

Kama tulivyotangulia kusema, hakika imani kama hizi hazihusiani na dini. Na labda hatuwezi kuthibitisha uhusiano wa ishara na athari au matokeo ya ishara hizo kisayansi. Lakini bila shaka, imani hizo ni sehemu ya utamaduni wa watu, na kila jamii aghalabu huwa na imani kama hizo. Huenda imani hizo zinalenga kuzuia wanajamii kutofanya mambo fulani ambayo wanayaona si mazuri kufanya, au ni jitihada ya kujaribu kueleza mambo au matokeo au hali wanazokutana nazo katika maisha ya kila siku.

## 3. Chakula

Katika sehemu hii tutaeleza mambo mbali mbali kuhusu chakula katika utamaduni wa Kiswahili ikiwa ni pamoja na aina au majina yake, wakati wa chakula, namna ya mapishi na adabu na miiko ya chakula.

### 3.1 Aina/majina ya vyakula

Hapa tutataja majina au aina za vyakula katika mafungu kama ifuatavyo; **a) Chakula**: Chakula hurejelea mlo mkuu kama vile; wali, ugali, mihogo, ndizi za kupika, pilau, biriani na viazi vya kupikwa. **b) Vitoweo**: Hivi ni jamii ya nyama ambayo huliwa pamoja na mlo mkuu kama vile; nyama ya kuku, ng'ombe, mbuzi, nyama ya kondoo, nyama ya porini na samaki. **c) Matunda**: Haya ni kama machungwa, maembe, mananasi, mapapai, zabibu, mapera, mabalungi, mafenesi, matufaha, mananasi n.k. **d) Vinywaji**: Hivi ni vimiminika kama vile; maji, chai ya rangi, chai ya maziwa, kahawa, soda, maji ya matunda/juisi n.k. **e) Vitafunwa**: Hivi ni vitu vinavyoliwa pamoja na kinywaji hasa asubuhi kama vile; sambusa, mkate wa kumimina, maandazi, chapati na mayai ya kuchemsha au ya kukaanga. **f) Mbogamboga**: Hujumuisha vitu kama; mboga za majani, kabichi, nyanya, karoti, pili pili boga, figili, bamia, biringanya na vitunguu. **g) Viungo**: Hivi ni vitu vinavyoongeza ladha katika chakula kama vile; chumvi, mbilimbi, nyanya, kitunguu saumu, tangawizi, pilipili, ndimu, hiliki, mchai chai, karafuu, pilipili manga, nazi n.k.

### 3.2 Wakati wa chakula

Kwa kawaida kuna milo mikuu mitatu. Mlo wa kwanza ni chakula cha asubuhi/chai/staftahi/kifungua kinywa. Mlo huu aghalabu huwa ni kinywaji kama chai inayoandaliwa kwa kuchemsha maji na kutia majani ya chai, sukari na viungo kama hiliki na mchaichai kwa *chai ya rangi* na ikiongezwa maziwa huitwa *chai ya maziwa*. Chai hunywewa pamoja na kitafunwa kama chapati, maandazi au vitumbua. Pili, ni mlo wa mchana; mlo huu huwa na chakula kikuu kama wali wa

nazi au ugali pamoja na kitoweo kama mchuzi wa kuku au samaki wa kukaanga pamoja na mboga mboga au viongeza ladha kama pilipili. Mlo wa mwisho ni chakula cha jioni (chajio), mlo huu aghalabu hufanana na ule wa mchana, lakini baadhi ya watu hupendelea kula vitafunwa kama chapati au mikate kwa mlo wa jioni pia.

### 3.3 Namna ya mapishi

Kuna namna kadhaa za kuandaa vyakula kama kwa kuchemsha, vyakula vya kuchemsha mfano wake ni kama supu ya kuku au samaki. Kuna vyakula vya kukaanga kwa mafuta kidogo hivi ni kama samaki wa kukaanga au mchuzi. Namna nyingine ni kuoka: vyakula vya kuoka ni kama mkate. Aghalabu zamani watu walitumia mkaa kuoka vyakula vya aina hii, siku hizi wengi wamehamia katika uokaji kwa majiko ya umeme au gesi. Vile vile kuna vyakula vya kubanika hivi ni kama samaki wa kubanika, mishikaki au nyama choma. Mwisho ni vyakula vya kukaanga katika mafuta mengi; vyakula hivi ni kama vile maandazi au kuku wa kukaanga.

### 3.4 Mambo ya kitamaduni yanayohusiana na chakula

Katika sehemu hii tunadondoa kwa ufupi mambo ya kitamaduni kuhusiana na chakula ikiwemo adabu na miiko ya chakula.

- Neno “chai” kitamaduni linatumika kwa maana sawa sawa na “kifungua kinywa/staftahi/ chakula cha asubuhi. Ni kawaida kusikia mtu akiuliza, “umeshakunywa chai?” na maana yake ni kutaka tu kujua kama umeshapata kifungua kinywa.
- Vyakula vya Kiafrika/Kiswahili kwa kawaida ni vya kukaanga, vyenye viungo, mafuta na sukari nyingi.
- Watu wanapoanza kula husema “*Bismillahi*” (ninaanza kwa jina la Mungu) na wanapomaliza kula husema “*Alhamdulillahi*” (ninamtukuza/ninamshukuru Mungu). Pia ni adabu kumshukuru mtu aliyekuandalia chakula k.v mama, mpishi, au mwenyeji wako kwa kusema “asante kwa chakula” naye atakujibu “karibu/bila asante/asante kwa kushukuru”.
- Kazi ya kuandaa/kupika chakula/kusafisha vyombo vya chakula ni kazi ya wanawake/watoto wa kike. Kitamaduni ni aibu kwa wanaume kuonekana na jamii wakifanya kazi hizo.
- Si adabu kabisa kutumia mkono wa kushoto wakati wa kula/kumpa mtu chakula.
- Watu hula kwa mkono (mkono wa kulia) na huosha mikono kabla na baada ya kula kama utamaduni hata kama wanatumia vijiko.
- Nyama ya nguruwe haiuzwi katika maduka ya kawaida ya nyama (buchani) au mikahawa ya umma, kwa sababu Waswahili wengi ni Waislamu na hawaruhusiwi kula nyama hiyo. Tafsida ya “kitimoto” hutumika ili kupunguza ukali wa neno “nguruwe”.

- Waswahili pia hawaruhusiwi kunywa pombe, kutokana na imani yao ya dini ya Kiislamu.
- Vyakula vikuu vinavyoutambulisha utamaduni wa Kiswahili ni kama vile; ugali, pilau, maandazi, chapati na kachumbari.
- Ni adabu kumaliza chakula unachopewa/unachojipakulia mwenyewe katika sahani yako, na si adabu kabisa kuchezea chakula.
- Si adabu kutoa sauti wakati wa kula au kuzungumza na chakula mdomoni.
- Nyama ya kuku ni maarufu kama chakula cha heshima kwa mgeni. Na ni ukarimu kumpa mgeni chakula au kinywaji anapokuja nyumbani kwako hata kama hakukujulisha ujio wake.
- Mgeni anapokaribishwa chakula si vizuri kukataa, ni muhimu kula japo kidogo "suna".
- Katika mapishi watu hawatumii vipimo kama gramu, au mililita, wapishi kwa kawaida hutumia makadirio tu kulingana na uzoefu wao. Kwa mfano husema, chumvi kidogo, kitunguu kimoja kidogo, vikombe viwili, kijiko kimoja cha chai n.k
- Hakuna utamaduni wa kugawa mlo katika awamu kama vile kwanza kifungua mlo (starter), mlo wenyewe (main course) na mwisho kitinda mlo (dissert). Vyakula vyote huwekwa mezani aghalabu kwa utaratibu wa chakula, kitoweo, matunda, kinywaji na viongeza ladha kama chumvi, pili pili, kachumbari, achari, mbilimbi n.k
- Ni heshima kuwapisha wageni/watu wazima/wazee/wakubwa/viongozi/wanaume kwanza wakati wa chakula, halafu wenyeji/wadogo/vijana/watu wa kawaida/wanawake baadaye.

**4. Mavazi**

Mavazi ni jambo linaloweza kuwatambulisha watu na ni sehemu ya utamaduni pia. Kwa mfano vazi la "sari" ni vazi la utamaduni wa Kihindi, vazi la "kimono" ni vazi la utamaduni wa Kijapani. Katika utamaduni wa Kiswahili, mavazi tunaweza kuyagawanya kulingana na jinsia, urasmi na adabu. Kuna mavazi ya kiume/ya wanaume kama vile kanzu, msuli, kofia, suruali, shati, na kaptula. Mavazi hayo isipokuwa kaptula na msuli ni mavazi ya heshima na yaweza kuvaliwa sehemu rasmi au nje ya nyumbani. Kaptula na msuli tunasema si mavazi rasmi kwa maana ya kuwa huwezi kuvaa sehemu rasmi kama kazini/ofisini. Kwa wanawake mavazi ya kike ni kama khanga, kitenge, baibui, gauni, sketi, na kilemba. Kwa wanawake mavazi ya heshima aghalabu ni yale yanayofunika sehemu kubwa ya mwili.

**4.1 Mambo ambayo si heshima (si Adabu) katika mavazi**

Si heshima/ si adabu kwa mwanamke/msichana kuvaa nguo fupi aghalabu iliyo juu ya magoti, kuvaa nguo inayobana sana, nguo ambayo inaonyesha (transparent), nguo inayoacha wazi sehemu kubwa ya kifua au mgongo, nguo yenye mpasuo mkubwa, nguo inayoacha wazi sehemu ya tumbo/

kitovu, nguo inayoonyesha nguo ya ndani (k.v chupi). Kwa wanaume, si adabu/si heshima kwa mwanaume kusuka nywele, kuvaa hereni, kuvaa suruali chini ya makalio, kuvaa kofia (*cap*) unapozungumza na mtu mzima/mzee/mtu unayemuheshimu au unapokuwa katika sehemu rasmi kama shuleni, au kazini.

### 4.2 Khanga

Miongoni mwa mavazi ya Kiswahili, vazi la khanga ni maarufu zaidi. Khanga ni aina ya kitambaa cha pamba chenye umbo la mstatili na hugawanywa katika sehemu tatu: Kwanza ni pindo yaani sehemu za ukingoni mwa khanga, pili ni mji yaani sehemu ya kati kati ya khanga, na sehemu ya tatu ni jina la khanga/msemo wa khanga aghalabu huwa sehemu ya chini ya khanga kabla ya ukingo wa chini wa khanga. Kwa kawaida khanga huwa na rangi ng'aavu na zilizokoza (*bright colours*) kama vile kijani, manjano, pinki, buluu, samawati n.k na huwa katika pea/jozi. Wavaaji hasa huangalia uzuri wa khanga kulingana na michoro na rangi ya khanga katika sehemu ya mji, na muhimu zaidi msemo wa khanga; katika sehemu inayofuatia tutafafanua zaidi kidogo kuhusu misemo ya khanga.

#### 4.2.1 Misemo ya khanga

Msemo au jina la khanga ni namna moja ya watu kufikisha ujumbe, watu husoma misemo ya khanga mtu avaapo khanga. Kuna misemo ya aina mbali mbali; kama vile misemo kuhusu Mungu kwa mfano: *Mshukuru Mungu kwa Kila jambo*. Misemo mingine hutukumbusha umuhimu wa mama au shukrani kwake kwa mfano; *Asante mama kwa malezi yako mema, Hakuna kama mama*. Kuna misemo ya kuonyesha furaha kama; *Furaha yako ni furaha yangu, Furaha ya harusi*. Vile vile misemo inayotaja methali za Kiswahili kwa mfano; *Elimu ni bahari, Usitukane mamba kabla hujavuka mto* na hata vijembe kama vile; *Pili pili ya shamba yakuwashiani? Jirani mbaya usimwonee haya* n.k.

#### 4.2.2 Matumizi ya Khanga

Khanga hasa ni vazi la wanawake. Khanga huvaliwa na rika zote kuanzia wasichana wadogo, watu wazima, hata wazee. Aghalabu kila mwanamke huwa na jozi kadhaa za khanga. Husemekana kama khanga ni vazi la mwanamke kutoka kuzaliwa mpaka kufa; Mtoto anapozaliwa hufunikwa khanga, anapofika rika la balehe pia huzawadiwa na kuvikwa khanga, anapoolewa vile vile huzawadiwa khanga na hata anapokufa jeneza lake hutambulika kwa kufunikwa khanga.

Khanga ina matumizi mengi sana; baadhi ya matumizi yake ni; Mosi, kufunga kiunoni hasa mtu anapokuwa nyumbani ni sawa na inavyotumika aproni jikoni katika tamaduni nyingine. Pili,

khanga mbili; moja ikiwa imefungwa kiunoni na ya pili ya kujitanda juu kutoka kichwani hadi kiunoni hutumika kama vazi la kuswalia kwa Waislamu. Tatu, wanawake wanapoenda katika misiba hujifunga au kujitanda khanga, hii ni kama namna ya kujisitiri au vazi la heshima. Nne, kama vazi la sherehe, watu wanapokwenda harusini aghalabu huweza kuwa na sare ya khanga hususan yenye maneno ya furaha. Tano, kama kilemba khanga hutumika kufunga kichwani kama kilemba hasa kwa wanawake. Sita, kama mbeleko; ni kawaida kuwaona akina mama wamewafunga watoto mgongoni kwa kutumia khanga. Saba, kama taulo; kitambaa cha khanga ni cha pamba kama tulivyokwisha kusema juu, hii hufanya khanga kuwa kitu muafaka wanachotumia watu kujifutia maji wanapotoka kuoga sawa sawa na litumikavyo taulo. Nane, kushona nguo; khanga hutumika kushonea nguo mbali mbali kama vile gauni/sketi. Tisa, kama nepi kwa mtoto mchanga; khanga kuu kuu huwa na sifa ya ulaini, aghalabu hukatwa katika vipande vidogo vidogo kiasi na kukunjwa katika umbo la pembe tatu tayari kwa kutumika kama nepi kwa mtoto. Siku hizi aghalabu watu walio mjini na wenye kipato hutumia nepi za kisasa za kutumia na kutupa (*diapers*), lakini bado desturi ya kutumia khanga inaendelea hasa vijijini na kwa watu wasio na kipato kikubwa. Mwisho, kumfunikia mtoto; khanga hutumika sana kumfunikia mtoto, hasa watoto pale wanapozaliwa. Khanga kuu kuu hutumika kwa sifa ya ulaini wake basi huonekana kama nguo rafiki kwa ngozi changa ya mtoto.

**5. Hitimisho**

Katika Makala hii tumeangazia vipengele vitatu zaidi vya utamaduni wa Kiswahili kupitia mada: *Utamaduni wa Kiswahili Juu ya Mambo yahusuyo Dini, Chakula, na Desturi za Mavazi*. Kwanza, tumefahamisha kuwa dini ni kipengele kinachoweza kutusaidia kuutambua utamaduni wa watu, na kuwa utamaduni wa Kiswahili unanasibishwa au umefungamana sana na dini ya Kiislamu kwani Waswahili waliathiriwa na ujio wa Waarabu waliokaa kwa muda mrefu katika pwani ya Afrika Mashariki wakiwasilimisha wenyeji, kujenga misikiti na kuwapa taathira za ustaarabu wa dini hiyo sambamba na kufanya biashara. Pia, tumefafanua kwa ufupi misingi ya Uislamu ni ipi, na kugusia baadhi ya mifano inayotuonyesha kuwa Waswahili wana itikadi zao nyingine za kimila ambazo si sehemu ya mila za dini ya Kiislamu. Pili, tumefafanua kipengele cha chakula na kudondoa mambo mbali mbali ya kitamaduni yahusuyo utamaduni wa chakula ikiwa ni pamoja na adabu na miiko yake. Tatu, tumeangazia desturi za mavazi, tukilipa nafasi zaidi vazi la khanga; vazi maarufu la wanawake na linaloutambulisha utamaduni wa Waswahili hususan wa Afrika Mashariki. Tumeangalia khanga ni nini? Inatumika wapi? Na nani? Wakati gani? Misemo yake n.k. Tumedhihirisha kuwa kwa wingi wa matumizi yake, vazi hili linatawala maisha ya mwanamke wa Kiswahili tangu kuzaliwa mpaka kufa: Tunaweza kusema, “khanga ni mwanamke na mwanamke ni

khanga daima hawaachani!"

Sawa sawa na makala zilizopita: "Makuzi *na Hatua za Maisha katika Utamaduni wa Kiswahili*" (Isack 2018:105-118) na "*Dhana na Dhima ya Familia na Unasaba katika Utamaduni wa Kiswahili*" (Isack 2019:259-269), makala hii inapendekezwa kwa wakufunzi na wajifunzaji wa Kiswahili kama Lugha ya Kigeni kwa lengo la kupunguza mwanya wa maarifa kutokana na uchache wa rejea zinazowalenga kundi husika. Pamoja na juhudi hizi, bado tunahitaji kuwa na rejea zaidi juu ya vipengele vingine ambavyo bado havijagusiwa katika maandiko yaliyopita. Miongoni mwa mada anazopendekeza mwandishi ni mambo yahusuyo lugha, fasihi, sanaa nyingine, burudani na ishara za mwili.

**Marejeo**

Farsi M.S

1960 *Kurwa na Doto. Maelezo ya Makazi katika Kijiji cha Unguja*, East Africa Literature Bureau, Nairobi.

Isack, Zainabu Kassu

2018 " Makuzi na Hatua za Maisha katika Utamaduni wa Kiswahili", katika *Frontier of Foreign Language Education 1, 105-118*.

2019 " Dhana na Dhima ya Familia na Unasaba katika Utamaduni wa Kiswahili", katika *Frontier of Foreign Language Education 2, 259-269*.

Mbaabu, Ireri

1985 *Utamaduni wa Waswahili*, Kenya publishing & Book Marketing Co. Ltd, Nairobi.

Mirza, Sarah & Strobel, Margareth

1991 *Wanawake watatu wa Kiswahili: Hadithi za Maisha kutoka Mombasa, Kenya*, Indiana University Press, Bloominton & Indianapolis.

Ndalu, Ahmed & King'ei Kitula G.

1994 *Kamusi ya Methali za Kiswahili*, East African Educational Publishers Ltd, Nairobi.

Taasisi ya Taaaluma za Kiswahili (TATAKI)

2014 *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (Toleo la Tatu), Oxford University Press, Nairobi.